HALIUZWI

NATIONAL HEALTH INSURANCE FUND
NHIF
Dedicated to providing quality health Care
ISO 9001:2015 CERTIFIED

# NHIF AFYA NJEMA

ISBN NO. 798-9987-9484 | TANZANIA | TOLEO LA 021 | SEPT. 2024



**Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan**
Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

## Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote ni Uhakika wa Matibabu kwa Wote

Namna NHIF ilivyojipanga kuanza utekelezaji wa Bima ya Afya kwa Wote .... **Uk. 08**

# JARIDA LA NHIF AFYA NJEMA

**BODI YA WAHARIRI**

**Mwenyekiti**
Anjela Mziray

**Mhariri wa Habari**
Grace Michael

**Wajumbe**
Celectine Muganga
Cosmas Mugasa
Victor Wanzagi
Rose Temba
David Sikaponda

**Msanifu**
Elisha D. Mwanjoka

# YALIYOMO

| | |
|---|---|
| TAHARIRI | 3 |
| NENO LA MKURUGENZI MKUU | 4 |
| SHERIA YA BIMA YA AFYA KWA WOTE NI UHAKIKA WA MATIBABU KWA WOTE | 6 |
| JIPANGENI UTEKELEZAJI WA BIMA YA AFYA KWA WOTE – KATIBU MKUU - AFYA | 10 |
| SITAVUMILIA UDANGANYIFU- MWENYEKITI BODI NHIF | 11 |
| MFUKO UMEENDELEA KUBORESHA HUDUMA KWA WANACHAMA, WATOA HUDUMA NA WANANCHI KWA UJUMLA | 14 |
| MAGONJWA SUGU YASIYOAMBUKIZA | 19 |
| NHIF YASHIRIKI BONANZA LA DODOMA | 20 |
| UJUE MPANGO WA HUDUMA ZA ZIADA ZA NHIF | 22 |
| UJUE UTARATIBU WA MAKAMPUNI BINAFSI KUJIUNGA NA NHIF | 23 |
| NHIF ILIVYONG'ARA SABASABA NA NANENANE | 26 |



# TAHARIRI

## TUJIANDAENI KUNUFAIKA NA BIMA YA AFYA KWA WOTE

Mapema Mwezi Novemba 2023, Bunge letu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lilipitisha Muswada wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote ambao tayari umepata baraka za Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye amesaini muswada huo na kuwa Sheria kamili.

Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote imetangazwa kuanza kutumika kupitia Tangazo la Serikali Na. 700A la Mwaka 2024. Kwa upande wa Kanuni za Bima ya Afya kwa Wote zimeandaliwa na kutangazwa kuanza kutumika kupitia Tangazo la Serikali Na. 809 la mwaka 2024 kwa lengo la kuwezesha utekelezaji wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote

Sheria hiyo ambayo imejaa manufaa mengi hususan katika eneo la wananchi kupata huduma za matibabu kwa kutumia mfumo wa bima ya afya ambao unamuwezesha kupata huduma wakati wowote na popote alipo nchini bila kuwa na kikwazo cha fedha.

Kwa kipindi kirefu kumekuwa na kilio cha gharama kubwa za matibabu ambazo wengi wa wananchi wameshindwa kuzimudu na kujikuta wakiingia kwenye umasikini kwa kuuza mali zao ili wapate fedha za kujitibia hivyo ujio au utekelezaji wa sheria hii unaondoa changamoto hizo kwa kuwa viwango vya kujiunga na bima ya afya ni nafuu.

Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote inaleta usawa wa wananchi katika kupata huduma za matibabu kwa kuwa imezingatia makundi yote likiwemo kundi la wananchi wasio na uwezo.

Katika kuhakikisha kundi la wananchi wasio na uwezo wanapata huduma, Serikali kupitia sheria hiyo, imeanzisha Mfuko maalum utakaogharamia huduma zao ikiwa ni pamoja na gharama za magonjwa yasiyoambukiza pamoja na ya dharura.

Suala la ubora wa huduma nalo limewekwa kisheria ambapo vituo vya kutolea huduma vitalazimika kuhakikisha vinatoa huduma bora kwa wananchi.

Kwa umuhimu wa sheria hii na manufaa yake, ni vyema sasa wananchi tuipokee na kuunga mkono juhudi za Serikali kwa kujiunga na Bima ya Afya kwa Wote ili tujihakikishie upatikanaji wa huduma za matibabu bila kikwazo cha fedha.

Pongezi nyingi pia kwa Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mhe. Dkt. Rais Samia Suluhu Hassan ambaye mara baada ya kuapishwa tu aliweka wazi msimamo wake juu ya suala la huduma za matibabu nchini na kuelekeza suala la bima ya afya kwa wote lifanyiwe kazi kwa haraka ambapo sasa matokeo yake yamejidhihirisha kwa sheria na kanuni kuanza kutumika.

**Bima ya Afya kwa Wote, Jiunge sasa.**

# Neno la Mkurugenzi Mkuu



**Dkt. Irene C. Isaka**
Mkurugenzi Mkuu - NHIF

## BIMA YA AFYA KWA WOTE

Kwanza kabisa nianze kuwashukuru sana wadau wetu wote hususan Wanachama na Watoa Huduma wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya kwa namna ambavyo mmeendelea kushirikiana na Mfuko katika hatua mbalimbali za uboreshaji wa huduma za matibabu kupitia ushauri na maoni yenu.

Aidha, nitumie fursa hii kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuniamini kuongoza Taasisi hii yenye dhamana kubwa ya utoaji wa huduma za matibabu na kwa Imani hii, naahidi nitafanya kazi kwa bidii, uaminifu na weledi mkubwa ili Mfuko uendelee kuimarika na kutoa huduma bora zaidi kwa Wanachama wake.

Kama mnavyofahamu, Mfuko umefanya maboresho mbalimbali ya kihuduma ambayo yote yalilenga kuimarisha na kurahisisha upatikanaji wa huduma kwenu hivyo tunawashukuru kwa kuyapokea na kushirikiana nasi katika kuyatekeleza. Kama Mfuko milango yetu iko wazi kwa ajili ya kupokea mrejesho, maoni na ushauri mbalimbali kwa lengo la kuboresha zaidi.

Mfuko unaendelea na utekelezaji wa majukumu yake huku ukiangalia uboreshaji wa maeneo mbalimbali ya kihuduma kwa kuzingatia uwezo wa Mfuko, mahitaji yaliyopo kwa wakati husika, Sheria, Miongozo na Taratibu zilizowekwa katika utoaji wa huduma za matibabu.


Wakati tukielekea utekelezaji wa Sheria ya Bima ya Afya kwa wote, Mfuko umejiandaa kuwahudumia wananchi wengi zaidi. maandalizi makubwa yaliyofanyika yamejikita katika maeneo ya TEHAMA inayojumuisha utambuzi wa wanachama wetu vituoni, usajili wa wanachama wapya pamoja na mifumo ya uchakataji na ulipaji wa madai.

Tumeendelea na usajili wa vituo vya kutolea huduma ambapo kwa sasa tunavyo jumla ya vituo 10,004 ambavyo viko katika mikoa yote ya Tanzania Bara na Zanzibar lakini pia tuna mtandao wa ofisi katika kila mkoa na sasa tunaendelea kusogea katika maeneo ya kimkakati ili kuweza kuwahudumia wananchi kiurahisi na kwa uharaka.

Niwaombe sana wadau wetu na wananchi kwa ujumla, wote kwa pamoja tuwe mabalozi wa kuhamasisha wananchi kujiunga na bima ya afya kwa kuwa ndio njia bora ya kupata huduma za matibabu bila ya kikwazo chochote.


199 www.nhif.or.tz nhiftz NHIFTanzania

ftz




## NHIF ni Mfuko wa Umma - ni wa kwetu sote.

1. Ulianzishwa kutuwezesha kupata matibabu kwa urahisi na uhakika kwa kuchangia kidogo kabla ya kuugua
2. Nikiugua fedha inatoka kwenye Mfuko huu kulipia matibabu yangu hata zaidi ya nilichokichangia
3. Ni jukumu langu kuulinda Mfuko huu

# SHERIA YA BIMA YA AFYA KWA MATIBABU KWA WOTE



## *Ndoto ya Bima ya Afya kwa Wote yatimia*

Kusainiwa kwa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote kunaleta matumaini makubwa kwa wananchi kwa kuwa utekelezaji wake utawezesha wananchi wote kupata huduma za matibabu bila vikwazo.

Sheria hii tayari imeshasainiwa na Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan baada ya kupitishwa na Bunge la Jamhuri ya Tanzania Novemba 2023 na sasa inasubiriwa kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali kwa ajili ya kuanza utekelezaji wake.

Kwa mujibu wa sheria hiyo, kila mwananchi atakuwa na uhuru wa kuchagua skimu ya bima ya afya na kujiunga nayo ili kumwezesha kupata huduma za matibabu wakati wowote anapohitaji.

Sheria hiyo inaweka Mfumo wa Bima ya Afya kwa Wote ambapo makundi mbalimbali yatajumuishwa ikiwa ni pamoja na Watumishi wa Umma na wa sekta binafsi, waliojiajiri wenyewe katika sekta isiyo rasmi na wananchi wasio na uwezo ambao sheria imeweka utaratibu wa kuwawezesha kuwa na bima ya afya.

Kuwepo kwa Sheria hii kuna faida ambazo hazikuweza kupatikana awali kutokana na kuwepo na wachache waliojiunga na kunufaika na hivyo kufanya kuwepo kwa kundi kubwa wasio nufaika. Sheria hii itawezesha uhakika wa matibabu kwa wote; kuimarisha uboreshaji wa huduma katika vituo vya kutolea huduma za afya vya Umma na binafsi, ikiwa ni pamoja na kuimarika kwa upatikanaji wa dawa, vitendanishi na vifaa tiba.

Manufaa mengine ni kuimarika kwa uhimilivu na ustahimilivu wa Skimu za bima ya afya kutoa huduma kwa kuwa wananchi watapaswa kuchangia kabla ya kuugua katika Skimu za Bima ya Afya.

Serikali imeshawekeza kwenye miundombinu ya afya. Kilichobaki ni wananchi sasa kuwa na uwezo wa kuzipata huduma hizo na Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote ndio suluhisho.
Kuna usemi unaosema "Afya ni mtaji" na katika



199 www.nhif.or.tz nhiftz NHIFTanzania

# WOTE NI UHAKIKA WA

- **Mhe. Rais Dkt. Samia aelezea manufaa yake kwa wananchi**
- **Aelezea uwekezaji uliofanywa na Serikali katika Sekta ya Afya**
- **NHIF yasema iko tayari na imejipanga kutekeleza, yampongeza Rais Dkt. Samia**



**Mhe. Jenista Mhagama (Mb)**
Waziri wa Afya

usemi huu unaweza ukauona ukweli wake moja kwa moja kwa kuwa hakuna mwananchi yeyote anayeweza kushiriki shughuli za maendeleo ya uchumi wa kifamilia na Taifa kwa ujumla bila kuwa na afya njema.

Kwa umuhimu huo, Serikali ya awamu ya sita chini ya Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan imeweka kipaumbele katika uwekezaji kwenye Sekta ya Afya hususan katika ujenzi wa vituo vya afya, ukarabati wa miundombinu na vifaa tiba vya kisasa na rasilimali watu hivyo kuwezesha upatikanaji wa huduma bora za matibabu kwa wananchi.

Uhakika wa upatikanaji wa huduma za matibabu kwa nchi yeyote ni kiashirikia kikubwa cha maendeleo ya nchi husika kwa wananchi wake kupata huduma bila ya kikwazo cha kifedha. Mfumo wa Bima ya Afya ni wa kisasa unaomwezesha mwananchi kupata huduma za matibabu wakati wowote anapozihitaji bila kuwa na kikwazo cha kifedha.

Hivi karibuni Mhe. Rais akiwa katika ziara mikoa ya Katavi, Rukwa na Songwe, amesikika mara nyingi akiwahamasisha wananchi kujiunga na Bima ya Afya ili waondokane na kukosa huduma za matibabu kutokana na kikwazo cha kifedha.
Kwa hatua yake, kama kiongozi wa nchi, amefanikiwa kuandaa mazingira bora ya upatikanaji wa huduma za matibabu kwa kuelekeza fedha nyingi katika sekta ya afya hivyo wajibu unabaki kwa wananchi kuchukua hatua stahiki ya kujiunga na bima ya afya.

Miongoni mwa juhudi hizo ni pamoja na hatua ya kupitishwa kwa sheria ya Bima ya Afya kwa Wote na kusainiwa ambayo inamtaka kila mwananchi kuwa ndani ya mfumo huo katika kupata huduma za matibabu.


Aidha, kitendo cha kila mwananchi kuwa ndani ya mfumo wa bima ya afya kitasaidia kupata huduma stahiki, kuepuka vifo vinavyoweza kusababishwa na kushindwa kumudu gharama za matibabu pamoja na kujiepusha kuingia katika lindi la umasikini kwa kuuza mali ili kupata fedha za kulipia gharama za matibabu.
Sheria hiyo ya Bima ya Afya kwa Wote, imeweka utaratibu wa kugharamia huduma za matibabu kwa kundi la watu wasio na uwezo kupitia mfumo wa bima ya afya baada ya utambuzi na usajili wa wananchi watakaokidhi vigezo ili kuhakikisha uhakika wa matibabu kwa kundi hilo la wananchi bila kikwazo cha kifedha.

Serikali katika Bajeti yake ya Mwaka 2024/2025 tayari imeainisha vyanzo vya mapato vitakavyogharamia kundi hili hivyo, utekelezaji wake kuwa na matumaini makubwa zaidi.

Mheshimiwa Rais Dkt.Samia amesema, Serikali imedhamiria kupeleka huduma bora za afya karibu na wananchi kwa kufanya uwekezaji katika hospitali zote nchini.

“Na tunaendelea kuweka mifumo madhubuti ya vyanzo vya uhakika vya fedha ili kutekeleza Bima ya Afya kwa Wote kwa wale wasiokuwa na uwezo kabisa, tutaweka utaratibu mzuri”.

“Serikali inatumia gharama kubwa na ili tuweze kwenda vizuri mahospitali mazuri yanajengwa, madawa yaendelee kuja, lazima Watanzania tuchangie kwenye huduma za afya kwa kujiunga na bima ya afya,” alisema Mhe. Rais.




Maafisa wa NHIF wakipita mtaa kwa mtaa kuelimisha wananchi kuhusu umuhimu wa kujiunga na bima ya afya.

# Maandalizi yaliyofanywa na NHIF katika kutekeleza suala hili

> *Tumeendelea kuboresha huduma zetu kwa kuongeza mtandao mpana wa vituo vya kutolea huduma kwa kutumia TEHAMA ili mwananchi anayejiunga na NHIF aweze kunufaika na huduma hizo*

Akizungumzia maandalizi yaliyofanywa na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya, Dkt. Irene Isaka amesema kuwa, kwa kutambua jitihada kubwa zinazofanywa na Serikali ya Awamu ya Sita, tayari Mfuko umeshafanya maandalizi ya kutosha ya kuhakikisha unahudumia wananchi wengi zaidi.

"Kwanza kabisa nimpongeze sana Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa namna alivyoweka nguvu katika suala la bima ya afya kwa wote, sisi kama mdau mkubwa katika kutekeleza suala hili tumejipanga na kwa sasa tumewekeza zaidi katika utoaji wa elimu hususan ya kuwaandaa wananchi kujua umuhimu wa bima ya afya na kujiunga," alisema Dkt.Isaka.

Akizungumzia utayari wa utoaji wa huduma kwa kundi kubwa la wananchi, amesema Mfuko umeimarisha mifumo yake ya TEHAMA



ili kuwezesha utambuzi wa wanachama, upatikanaji wa huduma kwa haraka wanapokuwa katika vituo vya kutolea huduma na malipo kwa watoa huduma kwa wakati.

"Tumeendelea kuboresha huduma zetu kwa kuongeza mtandao mpana wa vituo vya kutolea huduma ili mwananchi anayejiunga na NHIF, aweze kunufaika na huduma hizo kwa wakati anapozihitaji." Ameleeza.

Kutokana na hayo, ametoa wito kwa wananchi kujiunga na NHIF, kupitia Ofisi zilizoko kila Mkoa Tanzania Bara na maeneo ambayo Mfuko umekuwa ukiweka kambi za uhamasishaji wananchi.

"Ukiwa na kadi ya NHIF, una uhakika mkubwa wa kupata huduma wakati wowote na popote nchini, kwa upande wetu tumejipanga kuhakikisha tunawafikia wananchi kuwahudumia," amesisitiza Dkt. Isaka.

> *Ukiwa na kadi ya NHIF, una uhakika mkubwa wa kupata huduma wakati wowote na popote nchini, kwa upande wetu tumejipanga kuhakikisha tunawafikia wananchi na kuwahudumia*
>
> ***Dkt. Irene C. Isaka***
> *Mkurugenzi Mkuu - NHIF*



**Dkt. John Jingu**
Katibu Mkuu - Afya

# JIPANGENI UTEKELEZAJI WA BIMA YA AFYA KWA WOTE – KATIBU MKUU

Na Mwandishi Wetu, Arusha

Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya Dkt. John Jingu ameutaka Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), kujipanga na kuweka mikakati ya utekelezaji wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote ili kufanikisha matarajio ya ya Serikali na wananchi.

Hayo ameyasema hivi karibuni jijini Arusha wakati akizungumza na Wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi la NHIF waliokutana kuweka mikakati ya uboreshaji wa huduma kwa wadau wake.

“Jambo la Bima ya Afya ni kubwa, lazima tujipange vizuri katika utekelezaji wake, Sheria na Kanuni zimeshasainiwa na katika hili niwahakikishie Serikali iko na ninyi katika kila hatua ili muweze kufanikisha hili,” amesisitiza Katibu Mkuu.

Amesema kuwa ili kufanikisha suala hilo, Mfuko ujikite katika matumizi ya mifumo na kuongeza ubunifu katika vitita vyake ili kuleta ufanisi na tija katika utoaji wa huduma kwa wanachama wake.

Akizungumzia utendaji kazi, amewakata Watumishi kuwajibika katika maeneo yao kwa kutambua dhamana kubwa iliyowekwa na Serikali kwa Mfuko kuhudumia wananchi wake.

“NHIF mna dhamana kubwa sana na ni nguzo kubwa katika kuimarisha upatikanaji wa huduma za matibabu nchini, hakikisheni mnaboresha utendaji kazi wenu ili huduma mnazozitoa ziweze kwenda na wakati au mahitaji ya sasa,” amesema Katibu Mkuu.

Aidha, ametumia fursa hiyo, kuonya baadhi ya wanaojihusisha na vitendo vya udanganyifu na kuwataka kuacha mara moja na badala yake kuwa walinzi wa huduma ili Mfuko uendelee kuwa hai na kutoa huduma bora.

Katibu Mkuu amempongeza Mkurugenzi Mkuu Dkt. Irene Isaka kwa kuaminiwa na kuteuliwa na Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan kuiongoza NHIF ambayo ni taasisi nyeti na nguzo katika Sekta ya Afya.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mkuu, Dkt. Irene Isaka, amemhakikishia Katibu Mkuu kuwa watumishi wote wa Mfuko wako tayari kutekeleza Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote ili matarajio ya Serikali na wananchi yaweze kufikiwa.

“Tutafanya kazi kwa nguvu zote na weledi mkubwa, tumejipanga na tunafanya kazi kubwa kuweka mifumo yetu vizuri ili iweze kurahisisha utoaji wa huduma zetu,” alisema Dkt. Isaka.

***“Jambo la Bima ya Afya ni kubwa, lazima tujipange vizuri katika utekelezaji wake, Sheria na Kanuni zimeshasainiwa na katika hili niwahakikishie Serikali iko na ninyi katika kila hatua ili muweze kufanikisha hili”***
***Dkt. Jingu***


199 www.nhif.or.tz nhiftz NHIFTanzania

# SITAVUMILIA UDANGANYIFU- MWENYEKITI BODI NHIF



**Bw. Eliud Sanga**
Mwenyekiti wa Bodi - NHIF

Na Mwandishi Wetu, Arusha

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), Bw. Eliud Sanga amewaonya watumishi, watoa huduma, waajiri na wanachama wanaojihusisha na vitendo vya udanganyifu kuacha mara moja kwa kuwa bodi yake haitavumilia hilo.

Ametoa onyo hilo wakati akifungua Mkutano wa Baraza la Wafanyakazi la NHIF mjini Arusha hivi karibuni. "Kwa Watumishi wa Mfuko, wanachama na Watoa Huduma wasio waaminifu wanaojihusisha na udanganyifu waache mara moja, hatuna uvumilivu katika kuona yeyote akijinufaisha kupitia huduma zinazotolewa tunahitaji kuona Mfuko ukiwa hai na ukitoa huduma nzuri," amesisitiza.

Aidha, ameitaka Menejimenti kuhakikisha inaimarisha mifumo yake ya ndani ili iweze kubana mianya yote ya udanganyifu na iwezeshe utoaji wa huduma bora na kwa wakati.

Akizungumzia utendaji kazi wa Watumishi, amewataka kujipima wenyewe na kuhakikisha wanafanya kazi kwa bidii, weledi na kwa kuzingatia maadili na taratibu zote zilizopo na kuachana na tabia za kuweka makundi mahala pa kazi.

"Tusitengeneze makundi ndani ya Mfuko wetu, tengenezeni mfumo mzuri wa utendaji kazi ili muweze kutoa huduma bora kwa wadau wetu na matarajio ya Serikali yaweze kufikiwa," amesema Mwenyekiti wa Bodi NHIF.

Alitumia fursa hiyo kumpongeza Mkurugenzi Mkuu Dkt. Irene Isaka kwa kuaminiwa na Serikali kuiongoza NHIF ambayo ni taasisi nyeti yenye dhamana ya utoaji wa huduma za bima za matibabu.

Amewataka watumishi kumpa ushirikiano na kumtumia vizuri katika uboreshaji wa huduma kwa kuwa anao utaalam wa kutosha katika eneo la hifadhi ya jamii.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mkuu Dkt. Isaka, amemuahidi Mwenyekiti wa Bodi kuwa atasimamia Mfuko kwa weledi na uaminifu Mkubwa.

"Naomba kuweka wazi kwamba sina uvumilivu (zero tolerance) kwenye masuala ya udanganyifu na uzembe nitasimamia kuhakikisha tunaongeza wigo wa wanachama, tunatoa huduma bora kwa wanachama wetu. Nitasimamia matumizi ya TEHAMA, katika utendaji, tumeanza kubana matumizi ili tupunguze nakisi ya bajeti ya Mfuko. Pia tumedhamiria kuboresha mahusiano yetu na watoa huduma na wanachama wetu." Hivyo tutafanya upekuzi kwa watumishi wote na tutatoa mafunzo ya ndani (huduma kwa wateja, usajili, uchakataji madai, kupinga udanganyifu, matumizi ya mifumo, ununuzi na uwekezaji) kwa lengo la kuleta ufanisi" amesema Dkt. Isaka.

Akizungumzia maandalizi ya utekelezaji wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote, amesema Mfuko umeanza matayarisho hasa katika eneo la utoaji wa elimu kwa umma, mifumo itakayotumika katika kuandikisha wanachama, kukusanya michango na kuchakata madai.

"Tumeweka mipango yetu vizuri katika kutekeleza hili la bima ya afya kwa wote, tunajua matarajio ya Serikali katika jambo hili, hivyo nikuahidi kuwa tutafanya kazi kwa kujituma ili kufanikisha azma ya serikali" amesema Dkt. Isaka.


NATIONAL HEALTH INSURANCE FUND
NHIF
ISO 9001:2015 CERTIFIED
Taarifa za uanachama
Anuani za ofisi za NHIF nchi nzima
Taarifa za wategemezi wako
Vituo vya matibabu vilivyo karibu nawe
Orodha ya dawa na vipimo vilivyopo kwenye Kitita cha Mafao
NHIF Tanzania
JIPAKULIE
Huna haja ya kupata tabu, pata taarifa mbalimbali za uanachama wako kupitia
NHIF APP
ANDROID APP ON Google play
Available on the iPhone App Store

**Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan**
Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Matibabu ni gharama kubwa mno. Tusipochangia, huduma zitarudi nyuma. Tulipofika hapa, ili tuweze kutoa huduma endelevu; Suala la bima ya afya haliepukiki. Tujipange kila mmoja kuwa na bima yake ili tutibiwe ipasavyo'.

**10 Januari, 2024**



***Uhakika wa Matibabu kwa Wote***

# MFUKO UMEENDELEA KUBORESHA HUDUMA KWA WANACHAMA, WATOA HUDUMA NA WANANCHI KWA UJUMLA



Na Mwandishi Wetu

Huduma za matibabu ni moja ya huduma muhimu kwa kila mwananchi kwa kuwa ni huduma inayogusa afya na wakati mwingine uhai wa mtu husika. Kwa umuhimu huo, Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), umepewa dhamana ya kuhakikisha unasimamia utoaji wa huduma hizo kwa wanachama wake lakini pia kushiriki katika uboreshaji na umairishaji wa huduma katika vituo vya kutolea huduma za matibabu nchini kwa ajili ya wananchi wote.

Kwa sasa Serikali iko katika hatua za mwisho za maandalizi ya utekelezaji wa Sheria ya Bima ya Afya kwa wote, ili kila mwananchi aweze kuwa kwenye mfumo huo utakaomwezesha kupata huduma za matibabu bila kikwazo chochote. Hivyo, NHIF imejipanga kuhakikisha inawafikia wananchi wengi zaidi kwa kuwapa elimu, kuwahamasisha kujiunga na kuwasajili ili waanze kunufaika na huduma za matibabu.

Akizungumzia mikakati mbalimbali iliyowekwa, Mkurugenzi Mkuu wa NHIF, Dkt. Irene Isaka, ameelezea maeneo mbalimbali ambayo Mfuko umejipanga kuhakikisha unaboresha huduma zake na kuwawezesha wananchi kujiunga na kupata huduma bora.

**Matarajio**

Dkt. Isaka alianza kwa kuznugumzia matarajio ya Serikali ambayo ni kuona wananchi wake wote wanapata huduma za afya bila kikwazo cha fedha ambapo njia pekee na ya uhakika ni kwa kila mwananchi kuwa na bima ya afya. Katika hili NHIF ni mtekelezaji wa azma hiyo ya kuhakikisha kila mtanzania anakuwa na bima ya afya ili kuwa na uhakika wa matibabu.

"Katika kufanikisha hili, tumejipanga kutumia zaidi mifumo ya TEHAMA kuwarahisishia wananchi kujiunga na kupata huduma kuanzia ngazi ya zahanati hadi hospitali ya Taifa. Aidha, tumejipanga kutoa elimu kwa wananchi kupitia njia mbalimbali ili kumfikia kila mmoja hadi ngazi ya mtaa au kijiji.

"Vilevile tutaboresha mahusiano na wadau wetu wote ikiwemo sekta binafsi na kushughulikia malalamiko yote ndani ya muda mfupi ikiwa ni pamoja na kuweka mikakati ya kuepusha malalamiko kujirudia," amesema Dkt.Isaka.

**Maboresho yanayofanyika**

Mfuko umeendelea na uboreshaji wa huduma zake kila inapoonekana inafaa na bila kuathiri uhai na uendelevu wa mfuko. "Kwa sasa tunafanya maboresho makubwa ya mifumo yetu yatakayowezesha kurahisisha upatikanaji wa huduma kwa wanachama na watoa huduma."

Anaitaja mifumo hiyo ni pamoja na ya utambuzi wa wanachama, usajili, upokeaji na ulipaji wa madai pamoja na upatikanaji wa taarifa muhimu kwa wanachama na wadau wa mfuko.

Akizungumzia maboresho ya katika upande wa vifurushi vyake,

#nhiftz



199 www.nhif.or.tz nhiftz NHIFTanzania



amesema Mfuko umepanga kuja na vifurushi nafuu zaidi ya vilivyopo ili kumpa mwananchi uwezo wa kununua bima lakini pia kutumika kwa mpango wake wa Dunduliza kumwezesha mwananchi kuchangia bima kidogo kidogo na kuanza kunufaika baada ya kukamilisha lengo.

"Kwa upande wa uongezaji wa wigo wa huduma hatua hii itategemea matokeo ya tathmini zinazofanyika ambazo hushauri ni maeneo gani yafanyiwe maboresho hivyo, suala hili litakuwa ni endelevu. Aidha, tathmini mbalimbali zinaendelea kufanywa na endapo itaonekana kuna haja ya kuongeza huduma yoyote, itaongezwa kwa kuzingatia matokeo ya tathmini hizo." Amesema Mkurugenzi Mkuu.

**Mifumo Kidijitali**

"Kama nilivyodokeza hapo awali moja ya maboresho makubwa yanayoendelea kwa sasa ni eneo la mifumo ya utendaji, usajili wa wanachama utakuwa ni rahisi na kwa njia ya mtandao. Maboresho haya ya TEHAMA yatasaidia wananchi kuufikia Mfuko kwa haraka. Mabadiliko yanayofanyika kwa sasa yanalenga sio tu kuhudumia wadau kwa idadi iliyopo sasa, bali kuweza kuhudumia wananchi wote, chini ya utaratibu wa bima ya afya kwa wote."

Amesema, kupitia mifumo wanachama wanawezeshwa kujihudumia zaidi, kuanzia uandikishaji, ulipaji michango, ufuatiliaji wa huduma wanazopata na kujua vituo vinavyofanya kazi na huduma zinazotolewa katika vituo hivyo. Kadhalika, watoa huduma wanawezeshwa kuwasilisha madai yao kwa njia ya mtandao kwa haraka.

"Maboresho haya yatawawezesha watoa huduma na waajiri kuwasilisha taarifa, michango na kufanya usuluhishi kwa njia ya mtandao na wanapata taarifa mbalimbali zinazowahusu kwa wakati. Suala la uharaka na usahihi wa kuchakata madai ya watoa huduma limepewa uzito mkubwa" amesema Dkt.Isaka.

Mpango mwingine katika uboreshaji wa Mifumo ni kutumia Artificial Intelligence (AI), ili kuchakata madai na kutambua kwa urahisi viashiria vya udanganyifu. Kwenye utekelezaji wa haya, Mfuko utahitaji ushiriki watoa huduma kufanya mabadiliko stahiki kwenye mifumo yao, kwa viwango vilivyowekwa na Serikali, ili mifumo yao iweze kusomana na mifumo ya Mfuko kwa urahisi.



**Dkt. David Mwenesano**
**Mkurugenzi wa Tiba na Huduma za Kiufundi**

**NHIF na vituo vya afya vijijini**

Amesema, Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan katika mojawapo ya kazi kubwa iliyofanya ni pamoja na uboreshaji wa vituo vya kutolea huduma za matibabu ambapo hospitali zimejengwa na huduma zimeshushwa mpaka ngazi ya chini kabisa.

"Mfano mzuri huduma za kitalaam kwa sasa zinapatikana hadi ngazi ya hospitali za wilaya, hivyo kwa wanachama wa NHIF imekuwa ni habari njema sana kwao kutokana na urahisi wanaoupata katika kuzifikia huduma wanapozihitaji. Mfuko utaendelea kushiriki katika uboreshaji kwa kutoa mikopo nafuu kwa vituo vya afya ili viweze kuboresha mazingira ya kutolea huduma na kurahisisha upatikanaji wa dawa na vifaa tiba."





**Bi. Grace Michael**
**Kaimu Meneja Uhusiano**

**Maboresho mawasiliano**
Mfuko unazo njia mbalimbali za mawasiliano na wadau wake au upatikanaji wa taarifa zake. Njia hizo ni pamoja na barua pepe, tovuti, kurasa za mitandao ya kijamii, Kituo cha Huduma kwa Wateja ambacho hufanya kazi saa 24. Aidha Mfuko unayo Mobile App, ambayo wanachama na wale wasio wanachama wanaitumia kupata taarifa mbalimbali na kujipatia huduma zinazotolewa na NHIF bila kuhitaji kufika ofisini.

**Elimu kwa Umma**
Dkt.Isaka anasema, moja ya jukumu la NHIF ni kuhakikisha wananchi wanakuwa na uelewa wa dhana ya bima ya afya hivyo Mfuko kwa sasa unatekeleza mkakati wake wa masoko na elimu kwa umma ambapo unatumia njia mbalimbali za kutoa elimu ya bima ya afya.

"Mfuko umepanga kuendelea kutumia njia mbalimbali ikiwemo vyombo vya habari, mikutano ya hadhara, mikusanyiko mbalimbali kama kwenye masoko, maonesho, nyumba za ibada na mitandao ya kijamii kuwafikia wananchi popote walipo ili kuielewa dhana ya bima na wajiunge kabla ya kuugua."

**Ushirikiano na wadau wake**
Dkt.Isaka anasema, NHIF inafanya kazi kwa uwazi zaidi ikiwa shirikisha wadau wake katika hatua mbalimbali hususan zinazohusu maboresho ya huduma. Amesema kuwa milango ya Mfuko huwa wazi kwa mdau yeyote anayepata changamoto ya kihuduma ili aweze kutatuliwa na kuendelea kunufaika na huduma husika.

**Ushirikiano sekta binafsi**
Mfuko ni mdau mkubwa wa sekta binafsi katika kufanikisha azma ya Serikali ya bima ya afya kwa wote ambapo sekta hii imeajiri wafanyakazi ambao watakuwa na bima ya afya na pia inamiliki vituo ambavyo vinatoa huduma kwa wanachama wote wa Mfuko. Hivyo, Mfuko umepanga kuimarisha mahusiano na sekta binafsi na kuhakikisha kuendelea kufanya kazi kwa pamoja kwa maslahi ya pande zote.

**Mapambano dhidi ya rushwa na udanganyifu**
"Kwanza kabisa niseme kuwa, binafsi sina uvumilivu hata kidogo na yeyote awe Mtumishi au Mtoa Huduma au Mwanachama au Mwajiri atakayejihusisha na rushwa au udanganyifu. Kwa watumishi zipo taratibu za kiutumishi ikiwemo kufukuzwa kazi na taratibu zingine, kwa wanachama na watoa huduma ni pamoja na kufungia usajili wake au kadi ya matibabu na inapobidi kumfikisha katika vyombo vya sheria ili taratibu za mamlaka hizo zichukue mkondo wake.

Ameweka wazi kuwa katika masuala hayo atapambana kwa nguvu zote na kwa njia zote ili uhai wa Mfuko uwe endelevu uweze kutoa huduma kwa wananchi kama lilivyo lengo lake.

"Aidha, naenda kuimirisha mifumo ya udhibiti iliyopo kwa kuongeza udhibiti kwenye mifumo ya Tehama na kuimarisha Kitengo cha Kupambana na Makosa ya Udanganyifu," amesisitiza Dkt.Isaka.

**Changamoto zilizopo**
Changamoto kubwa iliyopo ni pamoja na uhiari wa wananchi kujiunga na kutoielewa dhana ya bima ya afya, kukithiri kwa vitendo vya udanganyifu kwa wadau ikiwemo baadhi ya wanachama, waajiri na watoa huduma.

Ili kukabiliana na changamoto hizi, Mfuko unaendelea kutoa elimu kwa wananchi kujiunga kwa wingi na huduma za bima ya afya kabla ya kuugua, kujiepusha na vitendo vya udanganyifu na kuweka mifumo ya kukabiliana na vitendo hivyo ili Mfuko uendelee kuwa hai na endelevu.





199 www.nhif.or.tz nhiftz NHIFTanzania

JIUNGE NA

# VIFURUSHI VYA BIMA YA AFYA

KWA UHAKIKA WA MATIBABU

## WEWE NA FAMILIA YAKO

## MICHANGO YA VIFURUSHI VYA NAJALI AFYA, WEKEZA AFYA NA TIMIZA AFYA



| NA. | UKUBWA WA FAMILIA | MCHANGIAJI KUANZIA MIAKA 18 - 35 | | | MCHANGIAJI KUANZIA MIAKA 36- 59 | | | MCHANGIAJI KUANZIA MIAKA 60+ | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | NAJALI AFYA | WEKEZA AFYA | TIMIZA AFYA | NAJALI AFYA | WEKEZA AFYA | TIMIZA AFYA | NAJALI AFYA | WEKEZA AFYA | TIMIZA AFYA |
| 1 | Mtu mmoja | 192,000 | 384,000 | 516,000 | 240,000 | 444,000 | 612,000 | 360,000 | 660,000 | 984,000 |
| 2 | Wanandoa | 384,000 | 732,000 | 996,000 | 456,000 | 864,000 | 1,188,000 | 684,000 | 1,284,000 | 1,908,000 |
| 3 | Wanandoa + Mtoto 1 | 504,000 | 924,000 | 1,272,000 | 576,000 | 1,068,000 | 1,464,000 | | | |
| 4 | Wanandoa + Watoto 2 | 612,000 | 1,116,000 | 1,536,000 | 696,000 | 1,248,000 | 1,728,000 | | | |
| 5 | Wanandoa + Watoto 3 | 720,000 | 1,284,000 | 1,788,000 | 804,000 | 1,416,000 | 1,980,000 | | | |
| 6 | Wanandoa + Watoto 4 | 816,000 | 1,452,000 | 2,028,000 | 900,000 | 1,584,000 | 2,220,000 | | | |
| 7 | Mtu mmoja + Mtoto 1 | 312,000 | 576,000 | 792,000 | 360,000 | 648,000 | 888,000 | | | |
| 8 | Mtu mmoja + Watoto 2 | 432,000 | 756,000 | 1,056,000 | 468,000 | 828,000 | 1,152,000 | | | |
| 9 | Mtu mmoja + Watoto 3 | 540,000 | 924,000 | 1,308,000 | 576,000 | 996,000 | 1,404,000 | | | |
| 10 | Mtu mmoja + Watoto 4 | 636,000 | 1,092,000 | 1,548,000 | 672,000 | 1,164,000 | 1,644,000 | | | |

NATIONAL HEALTH INSURANCE FUND
NHIF
Dedicated to providing quality health Care
ISO 9001:2015 CERTIFIED



# MAGONJWA SUGU YASIYOAMBUKIZA



Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza (MSY) ni magonjwa yanayompata mtu kutokana na njia zisizoambukizana kutoka kwa mtu mwingine kama ilivyozoeleka kwa magonjwa yanayotokana uambukizo. Kwa sasa MSY yamekuwa tishio na chanzo za vifo vingi duniani kwa zaidi ya asilimia 70.

**Magonjwa makuu yasiyoambukiza ni:**

1.Magonjwa ya moyo na mishipa ya damu,
2. Kisukari,
3. Saratani,
4. Magonjwa sugu ya njia ya hewa,
5. Magonjwa ya akili

**Visababishi vikuu vya magonjwa haya vinatokana kubadilika kwa mtindo wa maisha kama vile:**

1. Kutoshughulisha mwili
2. Lishe isiyozingatia misingi ya afya
3. Matumizi ya vilevi kupita kiasi
4. Matumizi ya tumbaku
5. Uzito kupita kiasi
6. Msongo

**Sababu nyingine ni:**

1. Uzee
2. Kurithi

Magonjwa yasipodhibitiwa husababisha madhara kwa mtu mmoja mmoja na kwa jamii nzima kwani yanahitaji matibabu maisha yote na kuzingatia masharti mahsusi. Kutokana matibabu ya maisha yote gharama za matibabu ni kubwa na huchangia umaskini kwa mtu mmoja mmoja, familia na jamii nzima.

**Bila kudhibitiwa, madhara yafuatayo yanaweza kutokea:**

1. Vifo vya umri mdogo
2. Kuathirika kwa ogani  na mifumo mingine ya mwili kama kufeli kwa figo, macho, mfumo wa fahamu, mfumo wa uzazi, n.k
3. Kiharusi
4. Ulemavu

Kwa kuwa “Kinga ni bora kuliko tiba”, ni vyema jamii ikachukua tahadhari na kujikinga na magonjwa haya hususani kwa visababishi vinavyotokana na kubadilika kwa mtindo wa maisha kwa kuzingatia yafuatayo:

1. Kuushughulisha mwili: kufanya mzaoezi angalau mara tatu kwa wiki kwa muda usiopungua dakika 30
2. Lishe inayozingatia misingi ya afya: wanga kiasi kidogo, protini kidogo, mboga mboga na matunda kwa wingi, kunywa maji ya kutosha angalau lita 2 kwa siku, n.k
3. Matumizi ya vilevi kwa kiasi mf. bia 2 kwa wanaume, bia 1 kwa wanawake
4. Kuacha matumizi ya tumbaku
5. Kujiepusha na msongo

# NHIF YASHIRIKI BONANZA LA DODOMA




Timu za NHIF za mpira wa miguu na mpira wa pete wameshiriki katika bonanza la Afya lililoshirikisha timu kutoka hospitali ya Mkoa wa Kagera (Kagera RRH) na hospitali ya Mkoa wa Dodoma (Dodoma RRH), bonanza hili lilifanyika mkoani Dodoma Julai 27 , 2024.

Michezo hiyo iliyojumiusha timu za Mpira wa pete (Netball), mpira wa Miguu (Football), kuvuta Kamba, kukimbia kwa magunia, na mpira wa wavu (Mpira wa Wavu) ikiwa na lengo la kupambana na magonjwa yasiyoambukisa, kuimarisha afya za watumishi, kuandaa timu za Mfuko kuelekea katika mashindano ya mashirika ya Umma (SHIMUTA) na kuimarisha mahusiano baina ya taasisi shiriki.

Aidha katika michezo hiyo Timu ya Mpira wa pete ya NHIF imeibuka mshindi wa kwanza wa kushika nafasi ya kwanza na kuchukua kikombe baada ya kuifunga timu ya Hospitali ya Dodoma goli 35 kwa 22, na kwa upande wa mpira wa Miguu timu ya Mfuko ikishika nafasi ya pili.

Hata hivyo,mabonza haya yatakua endelevu na lengo ni kuimarisha afya za watumishi na kupambana na magonjwa yasiyoambukiza na NHIF ni taasisi ya wananchi na katika mwendelezo kutakuwepo na ushiriki wa taasisi nyingine hata wananchi kwa sababu tunahusika na afya za wananchi.


199 www.nhif.or.tz nhiftz NHIFTanzania







## *Michezo ni Afya, Michezo ni Furaha*









**Bi. Anjela Mziray**
**Meneja Masoko na Huduma kwa Wateja**

# Ujue mpango wa huduma za ziada za NHIF

(Supplimentary Healthcare Services)

Ili kuhakikisha huduma bora za matibabu zinapatikana kwa wanachama wake, Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) umeanzisha mpango wa huduma za ziada kwa waajiri wanaohitaji huduma hizo.

Kwa kupitia mpango huu mwanachama anapewa fursa ya kuongeza huduma za ziada atakazopenda kulingana na mahitaji yake kwa makubaliano maalum kati ya mwajiri na NHIF.

Wanufaika wa mpango huu ni waajiri wote waliosajiliwa na NHIF

**Mwajiri anayo fursa ya kuchagua huduma za ziada kulingana na mahitaji yake. Huduma hizo ni pamoja na;**

- Matibabu ya nje ya nchi;
- Uchunguzi wa afya (medical checkup);
- Dawa zilizo nje ya kitita cha mafao;
- Gharama za ziada za miwani;
- Kulazwa katika wodi binafsi (private ward);
- Huduma za dharura na uokoaji kwa kutumia ndege au gari la wagonjwa (Air and Ground Ambulance); na
- Huduma za haraka za matibabu (Fast tracking services).

**Ili mwanachama aweze kunufaika na mpango huu mwajiri anahitajika kuwa na sifa na vigezo vifuatavyo;**

- Awe mwajiri aliyesajiliwa na Mfuko;
- Kuwasilisha fomu ya maombi kupitia mfumo; na
- Kulipa malipo ya ziada kwa ajili ya huduma hizo mwanzoni mwa mkataba.



# Ujue utaratibu wa Makampuni binafsi kujiunga na NHIF

Ili kuhakikisha kuwa kumekuwa na wigo mpana kwa wananchi kujiunga na huduma zake, Mfuko umeweka utaratibu wa usajili wa makampuni binafsi, ambapo usajili huu unafanyika kwa njia ya mtandao bima kulazimishwa kufika ofisini.

Mwajiri binafsi au Kampuni binafsi ili iweze kusajiliwa na kunufaika na huduma za Mfuko inatakiwa iwe imejiliwa na mamlaka za serikali zinazohusika na usajili.

**Mwajiri binfasi ili kusajiliwa na Mfuko anatakiwa kuwa na nyaraka zifuatazo;**

1. Awe na usajili wa kampuni kutoka katika mamlaka za Serikali.

2. Awe na wafanyakazi kuanzia 20 na kuendelea ambapo wanasajiliwa wote.

3. Awasilishe taarifa za wafanyakazi

4. Awe na Namba ya utambulisho wa mlipa kodi (TIN)

5. Awe amejiunga na Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) na NSSF.

6. Awe na anuani ya ofisi (physical address).

**Ili mwajiri/ kampuni binfasi kujiunga na huduma za Mfuko na kuwaunganisha wafanyakazi wake anatakiwa kujisajili kwa kufuata utaratibu ufuatao;-**

1. Ingia kwenye tovuti ya Mfuko ya www.nhif.or.tz

2. Usajili mtandaoni

3. Employer portal

4. Fungua akaunti kwenye mfumo wa employer portal

5. Ingia na kujaza taarifa za kampuni na wafanyakazi.


NATIONAL HEALTH INSURANCE FUND
NHIF
Dedicated to providing quality health Care
ISO 9001:2015 CERTIFIED
Jiunge na NHIF wewe na familia yako kwa Uhakika wa Matibabu




# JISAJILI KWA NJIA YA MTANDAO

Tembelea tovuti www.nhif.or.tz ujisajili

# NHIF ILIVYONG'ARA SABASABA NA NANENANE

- NHIF mnafanya kazi nzuri
  - **Mhe. Mazrui**

Waziri wa Afya Zanzibar Mhe. Nassor Mazrui ameupongeza Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), kwa kazi kubwa ya kuwahudumia wananchi na kuwafikia katika maeneo yao.

Mbali na hilo, amepongeza mashirikiano baina ya NHIF na Mfuko wa Huduma za Afya Zanzibar (ZHSF) yanayowezesha wanachama wa ZHSF kuhudumiwa katika vituo vilivyosajiliwa na NHIF Tanzania Bara.

Hayo aliyasema ndani ya Banda la NHIF katika Maonesho ya Sabasaba ya Kimataifa ya 48 katika viwanja vya Mwalimu Nyerere.

"NHIF mnafanya kazi nzuri sana katika utoaji wa huduma, mimi nimekuwa mwanachama wenu na nimefurahia huduma hivyo endeleeni kuwafikia wananchi kwa wingi zaidi ili wawe na uhakika wa kupata huduma za matibabu," alisema Mhe. Waziri.

NHIF katika maonesho haya inatoa huduma mbalimbali ikiwemo elimu, uhamasishaji, usajili wa wanachama wapya, kupokea maoni na kutatua changamoto za wanachama wanazokutana nazo wakati wa kupata huduma.




*NHIF mnafanya kazi nzuri sana katika utoaji wa huduma, mimi nimekuwa mwanachama wenu na nimefurahia huduma hivyo endeleeni kuwafikia wananchi kwa wingi zaidi ili wawe na uhakika wa kupata huduma za matibabu*




## *Mwanachama NHIF kupata huduma kwa kutumia namba ya NIDA*

Wanachama wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), hivi sasa wanaweza kupata huduma za matibabu kwa kutumia namba ya Kitambulisho cha Uraia (NIDA).

Kaimu Meneja kutoka Kitengo cha Mawasiliano NHIF, Bi Grace Michael amesema hayo katika maonesho ya Wakulima, Wafugaji na Wavuvi yaliyofanyika katika viwanja vya Nzuguni Jijini Dodoma.

Amesema mfuko huo umeendelea kurahisisha huduma zake hususan ya utambuzi wa mwanachama anapokuwa katika vituo vya kutolea huduma kwa kutumia namba hiyo ya NIDA.






"Kwa sasa mwanachama wa NHIF anaweza akatambuliwa kituoni kwa kutumia namba ya NIDA. Hii itaondoa changamoto kwa wale waliokuwa wanasahau vitambulisho nyumbani.

Hata hivyo huduma hii ni wanachama wote wenye umri wa miaka 18 na kuendelea, kwa mwanachama mchangiaji pamoja na watemegezi wake.

## JINSI YA KUPATA NAMBA YA MALIPO (CONTROL NAMBA) KWA WANAOHUISHA UANACHAMA WA VIFURUSHI VYA BIMA YA AFYA

1. Piga *152*00#
2. Chagua namba 2 - **Afya**
3. Chagua namba 1 - **NHIF**
4. Chagua namba 1 - **Mwanachama**
5. Chagua namba 4 - **Lipia Huduma**
6. Chagua namba 1 - **Michango**
7. Ingiza namba yako ya Uanchama/ namba ya kadi
8. Chagua namba ya herufi ya kwanza ya ofisi ya NHIF iliyo karibu nawe
9. **Chagua ofisi**
10. **Kubali**

***152*00#**

**Utapokea ujumbe wenye namba ya malipo kupitia simu yako**



# Je ni sahihi kumuazima mtu kitambulisho changu cha NHIF ili apate matibabu?

Hapana sio sahihi na ni kosa kisheria. Usiazime wala kutumia kitambulisho kisicho chako na hatua kali zitachukuliwa kwa wanaobainika.


NATIONAL HEALTH INSURANCE FUND
NHIF
Dedicated to providing quality health Care
ISO 9001:2015 CERTIFIED
#nhiftz
Piga
199
BURE
NAMBA YA KITUO CHA
HUDUMA KWA WATEJA
Tunakusikiliza saa 24 siku 7 za wiki
Uhakika wa Matibabu kwa Wote

# Anuani za Ofisi za NHIF

**MAKAO MAKUU**
Jengo la NHIF,
2 Barabara ya Ukaguzi,
S.L.P 1437,
41104 Tambukareli,
DODOMA.
Simu: +255 26 2963887/8
Barua pepe: info@nhif.or.tz

**ILALA**
Ofisi ya Mkoa wa Ilala,
Jengo la NHC,
Makutano ya Barabara ya Mirambo na Samora,
S.L.P 7195,
DAR ES SALAAM.
Simu: +255 22 2183797
Barua pepe: infoilala@nhif.or.tz

**GONGO LA MBOTO**
Ofisi ya Gongo la Mboto,
Ukonga, Jengo la Magereza Mkoa,
S.L.P 7195,
DAR ES SALAAM.
Simu: +255 737 221935
Barua pepe: infoilala@nhif.or.tz

**TEMEKE**
Ofisi ya Mkoa wa Temeke,
Kurasini Bendera Tatu,
S.L.P 45777,
DAR ES SALAAM.
Simu: +255 734 203163
Barua pepe: infotemeke@nhif.or.tz

**KIGAMBONI**
Ofisi ya Kigamboni,
Jengo la Kibada Gardens,
Barabara ya Mjimwema Kongowe,
Mtaa wa Kifurukwe,
S.L.P 45777,
DAR ES SALAAM
Simu: +255 734 203164
Barua pepe: infotemeke@nhif.or.tz

**KINONDONI**
Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF),
Ofisi ya Mkoa wa Kinondoni,
Jengo la PSSSF Commercial Complex,
Barabara ya Sam Nujoma,
S.L.P 32668,
DAR ES SALAAM.
Simu: +255 733 242199
Barua pepe: infokinondoni@nhif.or.tz

**UBUNGO**
Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF),
Ofisi ya Ubungo,
Jengo la Utawala, Ghorofa ya Pili
Stendi ya Magufuli - Mbezi,
Barabara ya Morogoro,
S.L.P 34562,
DAR ES SALAAM.
Simu: +255 733 242199
Barua pepe: infokinondoni@nhif.or.tz

**MOROGORO**
Ofisi ya Mkoa wa Morogoro,
Jengo la Kenya Commercial Bank (KCB), Ghorofa ya Pili,
Barabara ya Boma,
S.L.P 955,
MOROGORO.
Simu: +255 734 116860
Barua pepe: infomorogoro@nhif.or.tz

**DODOMA**
Ofisi ya Mkoa wa Dodoma,
Jengo la NHIF, Tambukareli,
Barabara ya Jakaya Kikwete,
Ghorofa ya Chini,
S.L.P 2221,
DODOMA.
Simu: +255 26 2963887/8, +255 737 708749
Barua pepe: infododoma@nhif.or.tz

**KIBAHA**
Ofisi ya Mkoa wa Pwani,
Jengo la Halmashauri ya Mji, Maili Moja,
S.L.P 30438,
KIBAHA – PWANI.
Simu: +255 735 445509, +255 734 130295, +255 734 130296
Barua pepe: infokibaha@nhif.or.tz

**TANGA**
Ofisi ya Mkoa wa Tanga,
Jengo la Old Revenue, Ghorofa ya Chini,
Mtaa wa Swahili,
S.L.P 5486,
TANGA.
Simu: +255 27 2645415
Barua pepe: infotanga@nhif.or.tz

**RUKWA**
Ofisi ya Mkoa wa Rukwa,
Jengo la NHIF,
Mtaa wa National Housing – Jangwani,
S.L.P 225,
SUMBAWANGA.
Simu: +255 25 2800358
Barua pepe: inforukwa@nhif.or.tz

**TABORA**
Ofisi ya Mkoa wa Tabora,
Jengo la Chuo cha Afya na Sayansi Shirikishi, Ghorofa ya Chini,
Barabara ya Kazehili,
S.L.P 1654,
TABORA.
Simu: +255 734 198580, +255 734 198582, +255 734 198583
Barua pepe: infotabora@nhif.or.tz

**KILIMANJARO**
Ofisi ya Mkoa wa Kilimanjaro,
Jengo la NSSF,
Makutano ya Barabara ya Old Moshi na Bath/Upinde,
S.L.P 8998,
MOSHI – KILIMANJARO.
Simu: +255 27 2755143, +255 27 2754264
Barua pepe: infomoshi@nhif.or.tz

**ARUSHA**
Ofisi ya Mkoa wa Arusha,
Jengo la NSSF Kaloleni Plaza,
Ghorofa ya Pili,
S.L.P 16110,
ARUSHA.
Simu: +255 27 2520026, +255 27 2520027
Barua pepe: infoarusha@nhif.or.tz

**RUVUMA**
Ofisi ya Mkoa wa Ruvuma,
Jengo la CWT, Ghorofa ya Pili,
Mtaa wa Zanzibar,
S.L.P 160,
SONGEA.
Simu: +255 25 2602908, +255 737 917889
Barua pepe: inforuvuma@nhif.or.tz

**KAGERA**
Ofisi ya Mkoa wa Kagera,
Jengo la Chama cha Walimu (CWT), Ghorofa ya Chini na ya Pili
Mtaa wa Mayunga Na. 11,
S.L.P 1950,
BUKOBA.
Simu: +255 28 2221193, +255 736 120740
Barua pepe: infokagera@nhif.or.tz

**SINGIDA**
Ofisi ya Mkoa wa Singida,
Jengo la NHC Singidani Complex,
Barabara ya Arusha,
S.L.P 762,
SINGIDA.
Simu: +255 26 2502236
Barua pepe: infosingida@nhif.or.tz

**KIGOMA**
Ofisi ya Mkoa Kigoma,
Jengo la NHC Biashara House, Ghorofa ya Pili,
Barabara ya Lumumba,
S.L.P 1165,
KIGOMA.
Simu: +255 28 2802650
Barua pepe: infokigoma@nhif.or.tz

**MARA**
Ofisi ya Mkoa wa Mara,
Jengo la NHC, Ghorofa ya Kwanza,
Makutano ya Mtaa wa Ghandhi na Kusaga,
S.L.P 1348,
MUSOMA.
Simu: +255 28 2620554
Barua pepe: infomara@nhif.or.tz

**IRINGA**
Ofisi ya Mkoa wa Iringa,
Jengo la NHIF,
Barabara ya Mapinduzi - Gangilonga,
Jengo la NHIF,
S.L.P 2486,
IRINGA.
Simu: +255 26 2701276
Barua pepe: infoiringa@nhif.or.tz

**MBEYA**
Ofisi ya Mkoa wa Mbeya,
Jengo la NHIF Tower,
Barabara ya Karume,
Ghorofa ya Kwanza,
S.L.P 6137,
MBEYA.
Simu: +255 25 2500656
Barua pepe: infombeya@nhif.or.tz

**ZANZIBAR**
Ofisi ya Zanzibar,
Jengo la Makao Makuu ya ZIC,
Ghorofa ya Nne,
Barabara ya Ali Hassan Mwinyi,
S.L.P 4888,
ZANZIBAR.
Simu: +255 24 22372247,
Fax: +255 24 22372242,
Barua pepe: infozanzibar@nhif.or.tz

**MANYARA**
Ofisi ya Mkoa wa Manyara,
Jengo la BAWASA, Mkabala na TRA,
Ghorofa ya Kwanza,
S.L.P 430,
BABATI - MANYARA.
Simu: +255 27 2510022
Barua pepe: infomanyara@nhif.or.tz

**LINDI**
Ofisi ya Mkoa wa Lindi,
Jengo la CWT, Ghorofa ya Kwanza,
Mtaa wa Msonobalini,
S.L.P. 51,
LINDI.
Simu: +255 23 2202901
Barua pepe: infolindi@nhif.or.tz

**SIMIYU**
Ofisi ya Mkoa wa Simiyu,
Jengo la Nsagali,
Mtaa wa Salunda,
S.L.P 471,
BARIADI – SIMIYU.
Simu: +255 738 160182
Barua pepe: infosimiyu@nhif.or.tz

**KATAVI**
Ofisi ya Mkoa wa Katavi,
Jengo la NHC,
S.L.P 223,
MPANDA - KATAVI.
Simu: +255 25 2820147
Barua pepe: infokatavi@nhif.or.tz

**NJOMBE**
Ofisi ya Mkoa wa Njombe,
Jengo la NSSF - Mafao House,
Mtaa wa Nazareth, Barabara ya Songea,
S.L.P 1085,
NJOMBE.
Simu: +255 26 2782199
Barua pepe: infonjombe@nhif.or.tz

**GEITA**
Ofisi ya Mkoa wa Geita,
Majengo ya Halmashauri (W) Geita,
Mtaa wa Bomani,
S.L.P 482,
GEITA.
Simu: +255 28 2520170
Barua pepe: infogeita@nhif.or.tz

**MWANZA**
Ofisi ya Mkoa wa Mwanza,
Jengo la TMDA, Ghorofa ya Pili,
Nyakato Buzuruga,
S.L.P 1187,
MWANZA.
Simu: +255 28 2981299
Barua pepe: infomwanza@nhif.or.tz

**SHINYANGA**
Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF),
Ofisi ya Mkoa wa Shinyanga,
Jengo la NSSF,
Barabara ya Mwanza,
S.L.P 230,
SHINYANGA.
Simu: +255 28 2763708
Barua pepe: infoshinyanga@nhif.or.tz

**MTWARA**
Ofisi ya Mkoa wa Mtwara,
Jengo la Raha Leo Complex, Ghorofa ya Tatu,
Barabara ya Chikongola,
S.L.P 484,
MTWARA.
Simu: +255 657 249342, +255 752 524255, +255 685 272878
Barua pepe: infomtwara@nhif.or.tz

**SONGWE**
Ofisi ya Mkoa wa Songwe,
Jengo la CWT,
Old Vwawa,
S.L.P 186,

SONGWE.
Simu: +255 25 2580157
Barua pepe: infosongwe@nhif.or.tz




# Bima ya Afya kwa Wote, Jiunge Sasa